
MIFUMO
ya
MAFANIKIO
NEW!
Ombea Mifumo Yako Kabla Adui
Hajakuwahi
Livingstone A Musa

# MIFUMO YA MAFANIKIO.

**Ombea Mifumo Ya Mafanikio Yako Kabla Adui Hajakuwahi.**

© May, 2025.

**LIVINGSTONE ANDERSON MUSA.**

# Mawasiliano:

**Kawaida: 0782 639 761 & 0621 669 761**

**Whatsapp: 0715 374 445**

**Email: livingstonemusa761@gmail.com**

**Facebook:** Superstone Chidebe II

**Instagramu:** Superstone95

**Tik tok:** Superstone 99

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA.**

*Hairuhusiwi kutoa nakala sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile iwe kupiga picha, kunakili, kupiga kopi au kusambaza bila idhini ya mmiliki wa kitabu hiki, isipokuwa kwa kunukuu kuliko ruhusiwa kisheria, kwa yeyote atakaye bainika kufanya kinyume hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.*

**ISBN: 978-9912-42-725-9**

Kazi ya kusanifu jalada na kupanga kitabu imefanywa vizuri na **Stoney Products,** +225 715 374 445,

Barua pepe livingstonemusa761@gmail.com

**© May, 2025**

# SHUKRANI.


Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mungu wangu wa mbinguni, kwa kunistahilisha kusiko sitahili katika maisha yangu, amenipa uzima, afya njema, familia nzuri, Amani, furaha, hekima na Upendo.

Kipekee kabisa nipende kuishukuru familia yangu ya Mzee Anderson na Bibi Mary Baladiga kwani muda mwingi imefanyika baraka kwangu, kunipa nguvu pale napohisi kuchoka, Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kwa nafasi ya upekee kabisa nipende kumshukuru mke wangu kipenzi Paulina Yoram kwa kunipa muda wake mwingi kuweza kuikamilisha kazi hii, amekuwa mshauri mzuri na mvumilivu pale nilipotumia muda wake katika kuandaa kazi hii hakulalamika badi aliendelea kunitia moyo, Mungu akubariki sana.

Nipende kutoa shukrani za dhati kabisa kwa: Elimon Chidabile, Gift Mbembati, Anord Sanga, Severino Lubugo, Johanes J Ryoba, Moses Shija pamoja na wanakikundi cha Mlowa Bwawani 2018 kwa mchango wao mkubwa kuanzia kitabu cha kwanza cha NJIA NILIZOPITA hadi sasa, ushauri wao na maoni yao yamenisaidia kusonga mbele.

Ninakushukuru msomaji wangu ambaye umekuwa nami bega kwa bega kufuatilia makala na vitabu vipya, bila kukusahau wewe msomaji wangu mpya, Mungu awabariki sana kwa zawadi ya muda wenu.




*Picha ya pamoja na Dk. Tulia Ackson ambaye ni Rais wa umoja wa mabunge duniani, Spika wa bunge la Jamhuri ya muungano wa Tanzania, mbunge wa Mbeya mjini, na mkurugenzi wa taasisi ya Tulia Trust (14 disemba, 2024).*

**“Hakuna zawadi yenye thamani kwangu kama kupewa muda”.**

# YALIYOMO.

**UTANGULIZI:** ………………………………………X

**SURA YA KWANZA:** Mashujaa walishinda vita …. 1

Hatima yako imebebwa na Mungu ………………… 13

Mifumo na Nidhamu ni Moyo na Damu …………… 15

**SURA YA PILI:** Aina kuu tano za mifumo ya mafanikio………………………………………… 22

**SURA YA TATU:** Kuwa wewe halisi ……………… 34

Mawe 15 ndani ya kombeo moja …………………… 37

Hakikisha wanakuelewa, hakikisha hawakuelewi…… 48

**SURA YA NNE:** Nguvu ya zawadi ………………... 59

Pongezi lake, nguvu yako……………… …………... 63

**SURA YA TANO:** Mambo 11 yanayoweza kuua kabisa mfumo wa mafanikio yako ……………………………………………… 65

Kupotezwa, kujipoteza, kujitafuta nakujipata… …… 81

**Hitimisho** ……………………………………… 87

**Marejeo** ………………………………………… 90

Kuhusu mwandishi ……………………………….....91

# UTANGULIZI.

Ni ukweli usiopingika kwamba hapa duniani kila unayemuona anatamani sana kufanikiwa, lakini tunatofautiana katika vipaumbele na aina ya mafanikio kama vile kielimu, kiuchumi, kiroho, kifamilia n.k

Hata wewe najua unatamani sana kufanikiwa katika maeneo yako muhimu.

Pamoja na shauku hiyo ni wachache wanaoweza kupata mafanikio halisi (mafanikio ya kusudi la Mungu ndani yao) na kundi kubwa linabakia katika mafanikio yasiyohalisi.

Mafanikio yanahitaji watu wenye msuli mkubwa katika kuyatafuta na msuli huo ni pamoja na: kutambua kusudi la kuumbwa kwako, malengo, vipaumbele, mikakati, nidhamu, bidi, uvumilivu n.k

Tutaenda kuangalia baadhi ya vitu muhimu ambavyo vimekuwa vikikosewa / kupuuzwa katika kutafuta mafanikio.

Chukua dakika chache jiulize unaelewa nini kuhusu neno "MAFANIKIO".

Kwanini kila mtu, hata wewe unataka kufanikiwa?

Ukishafanikiwa ili iweje?

Kumbuka: Ili ufanikiwe lazima ujue kusudi la Mungu ndani yako kwani litakusaidia kukuamulia:

- ✓ Kazi ya kufanya,
- ✓ Vipaumbele
- ✓ Ustawi wako
- ✓ Mke/mume wa kuishi nae

- ✓ Kazi ya kufanya
- ✓ Mazingira ya kuishi
- ✓ Hatima yako.

Neno mafanikio limekuwa na tafsiri tofauti, lakini 70% ya watu ukizungumzia Mafanikio akili hufikiri kuhusu kuwa na fedha nyingi, magari, kampuni na biashara nyingne.

**Mtu aliyefanikiwa ni yupi?**

1. Mwenye fedha nyingi?
2. Mwenye mali nyingi?
3. Mwenye Furaha na Amani maishani mwake?
4. Mwenye Kutambua kusudi lake LAKINI bado haliishi?
5. Mwenye kujua kusudi lake na ANALIISHI?.

**Mifumo ya mafanikio** ya mwanadamu hapa duniani imefungwa katika vitu vinne vikuu ambavyo ni Nidhamu, Uhusiano (connection), Juhudi, Kipaji na Bahati.

Hivyo ili uweze kuijua mifumo yako lazima ujue upo katika fungu lipi, je una kipaji kitakachokutoa kimaisha? Kama huna jiulize ndani yako kuna bidii / juhudi ya kufanya kazi?

Kama vyote viwili havipo jiulize tena, je wewe una konekisheni gani? Kama napo huna jiulize unabahati gani katika maisha?

Na katika vyote kikuu ni nidhamu, hata uwe na vitatu kati ya hivyo bila ya nidhamu ya hicho kitu bado si kitu.

Pamoja na kwamba kuna watu wana bahati sana na vitu vizuri kama karama, fedha, mali, marafiki wazuri nakadharika lazima ukae kwa

tahadhari kubwa kwamba huwezi kaa sehemu moja ukiisubiri bahati yako ije.

Msingi mkuu wa mifumo ya mafanikio yetu imejengwa katika Uhusiano (Konekisheni) ya asili (Mungu aliyehai) kabla ya kuzaliwa pamoja na juhudi baada ya kuzaliwa.

Na kila mmoja anatakiwa kuiombea mifumo ya mafanikio yake kwani kila kinachoonekana kilianzia katika ulimwengu usioonekana, kwa maana nyingine mafanikio yoyote huanzia ndani kwenda nje na si nje kwenda ndani.

Mafanikio yametafsiriwa kwa mitazamo tofauti na baadhi ya watu. Baadhi ya mitazamo yao kuhusu mafanikio ni kama ifuatavyo:

**“Mafanikio ni shauku ya kiulimwengu”**

**David Oyedepo.**

**“Huwezi kuwa na mafanikio zaidi ya ufahamu wako wa kusudi lililokuleta duniani”**

**Joel Nanauka.**

**“Njia pekee ya kuyafikia mafanikio ya kweli ni kujitoa kikamilifu kuihudumia jamii”**

**Aristotle**

**“Mtu aliyefanikiwa kweli ni yule anayeliishi kusudi la Mungu”**

**Adriano Mkonda.**

**" Ili kuwa mtu aliyefanikiwa ni lazima awe ni mtu wa matokeo chanya au endelevu kwake yeye na katika jamii yake na si vinginevyo"**

# TABARUKU.

Kitabu hiki ni heshima maalumu kwa wanangu **Patrick** pamoja na **Charity.**

01 **SURA YA KWANZA**

# MASHUJAA WALISHINDA VIKWAZO.

**Mfumo:** Ni njia inayowezesha kitu kufanya kazi, kama ulivyo mwili wa binadamu umeundwa kwa mifumo mbali kama vile mfumo wa mkojo, mfumo wa damu, mfumo wa mmeng'enyo wa chakula, mfumo wa uzazi mfumo wa moyo na kadhalika. Hii mifumo yote hutegemeana katika utendaji kazi ili mimi na wewe tuweze kuishi.

Vile mimea nayo inategemea mifumo mbali ili iweze kuishi, mifumo kama vile mfumo wa maji kutoka ardhini.

**Mifumo:** Wingi wa mfumo ikiwa na maana ili ufanikiwe katika eneo lolote kimaisha basi kuna mifumo tofauti iliyoungana kuifanya leo yako kuwa bora kuliko jana.

**Mafanikio:** Ni matokeo ya mwisho kabisa ya kuanguka kwingi, kukataliwa, kunyanyapaliwa, kuumizwa, kuvunjwa moyo, kukosolewa pamoja na majaribio ya kukata tamaa. Mafanikio hayaji kwa usiku mmoja isipokuwa umpitia baadhi mambo au yote yaliyoorodheshwa kwenye maana ya mafaniko.

**Success** *"is the ability to go from one failure to another with no loss of enthusiasim"* Winston Churchill.

**Mafanikio** si kuwa bora kuliko mwingine, bali ni kuwa bora kuliko ulivyokuwa jana “Hamisa Mobetto kupitia mtandao wake wa instagram. Na hi indo maana halisi na nyepesi ya mafanikio.

Wewe ni wewe njia alizotumia mwenzako kufanikiwa haziwezi kuwa zako, Mfumo wa mafanikio ni wewe mwenyewe.

**Kamwe huwezi kuwa kama mtu fulani (wewe ni wewe).** Angalia vidole vya mikono yako, kuna kifupi sana, kifupi cha wastani, kuna kirefu, kuna kirefu zaidi na kuna kifupi halafu kinene. Vivyo hivyo katika maisha ya kila siku tumegawanyika katika makundi tofauti baadhi ni kama haya:

**1. Kimaumbile na mwonekano.**

Kuna warefu, wafupi, wembamba, wanene, weupe, weusi, maji ya kunde n.k

**2. Uchumi.**Kuna matajiri (wenye kipato kikubwa), kuna wenye kipato cha wastani na kuna maskini (wenye kipato kidogo) lakini kuna mafukara.

**3. Hali ya maisha**

Kuna yatima, wajane, wagane, wanandoa (waliooa na kuolewa), tena pana utofauti kati ya kufa, kufariki na kuuwawa japo vyote huelezea tendo la kutoweka kwa uhai wa kiumbe hai.

**4. Hali za vyeo.**

Wachungaji, mapadri, masheikh, wanasiasa (rais, mawaziri, makatibu, mabalozi, wabunge, madiwani n.k) waandishi, mainjinia, maafisa, waalimu, wanasheria, madaktari, marubani, wakutubi n.k.

Wengi tunashindwa kufikia mafanikio yetu ya muda mrefu kwa sababu tunajaribu kuiga mifumo ya wengine kufanikiwa.

Unaweza kuona namna ambavyo watu wengi wakiona mwingine kafanikiwa kupitia mziki, hata kama alikuwa hapendi mziki basi mtu huyo jitihada zote atazihamishia huko akiamini kwamba nayeye atafanikiwa kupitia mziki, hili ni kosa kubwa Sana. Na hii ni sawa na kubeti. Tena hata sehemu zinamaana kubwa sana kama mifumo ya mafanikio, kuna mtu akiwa mkoa fulani au kijijini anafanikiwa zaidi kuliko akiwa mjini, na mwingine kinyume cha hapo. Jiulize kaanani yako ya mafanikio ipo wapi?

*“Ati kwa sababu MC fulani anatengeneza fedha nyingi kupitia comedi na wewe ukawe comedian na MC. Kila mmoja anacho kitabu cha historia ya maisha yake na haitakiwi kuwaza kwamba njia ya mtu fulani nawewe ndio iwe njia yako”.* Aliandika Mwijaku kupitia ukurasa wake wa facebook.

Mafanikio ya watu tuliokuwa nao zamani, tuliomaliza nao shule au vyuo, au mlishawahi kuwa katika daraja moja la maisha inapotokea mwingine kavuka daraja lile na mwingine bado mara kadhaa watu wengi wamejikuta wakitoka kwenye mifumo yao ya mafanikio, mara tu walipoona wenzao wamefanikiwa kabla yao, wengi huanza kulazimisha pre - mature exposure (Kuonekana kabla ya wakati) na kusahau kwamba tunatofautiana sana katika maeneo mengi.

Hata katika maandiko matakatifu ile barua ya Mtume Paulo kwa **2 Wakorintho 12: 5** “Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule” Paulo alikuwa akiwaeleza watu hawa kwamba huduma zipo nyingi, karama zipo nyingi wengine waliitwa kuwa waalimu, wengine manabii, wengine matendo ya miujiza, mwingine uwezo wa kufasiri ndoto n.k.

Vivyo hivyo kuna mifumo tofauti ya kufikia mafanikio lakini maana halisi ya mafanikio ni ile ya kwamba Ni hali ya kuwa bora kuliko jana. Hiyo ndiyo maana halisi ya mafanikio na si kuwa bora kuliko mwingine.

Simaanishi kwamba upunguze juhudi zako katika kupambania ndoto yako hapana, pambana na linalowezekana kufanyika lifanye katika njia iliyohalali, usitumie njia haramu kuyafikia mafanikio yako hiyo ndiyo kutaka kuonekana kabla ya wakati sahihi.

**Mhubiri 3: 1 – 8**, mhubiri mwana wa Daudi anaelezea namna kila jambo lina wakati wake sahihi.

Na ndiyo maana ulipokuwa mtoto ulianza na hatua kama vile kutofanya lolote, kukaa, kutambaa, kutembea kisha kukimbia na hapa kuna baadhi ya vitu hukuruhusiwa kuvifanya kabisa bila ridhaa ya wazazi au walezi wako lakini ulipokuwa mkubwa utaratibu ulibadilika kwa asilimia kubwa.

➢ Tambua kuwa hatua yako ya tatu (3) inaweza ikawa hatua ya kwanza kwa mtu mwingine.


Yaani kwenye kile kinachokukosesha usingizi, kuna mwenzako anakiona takataka, ndiyomaana kamwe usitamani kuwa na maisha ya mtu fulani kwa sababu hujui upande wake wa pili (upande wa maumivu) anayoyapitia na ukaiishia kuangalia ule uzuri tu unaoonekana. Kwani mara nyingi watu hupenda kuona mafanikio ya mtu lakini wasitake kujua maumivu, maanguko, uvumilivu, dharau, fedheha na kukatishwa tamaa na mambo mbali kabla ya mafanikio hayo, raiti wangekuwa wanaweka wazi kuna mtu usingemtamania maisha yake.

➢

- Kile kinachokukosesha usingizi kukipata, kwa mwingine ni jambo la kawaida sana.
- Hela yako ya kuchimbia dawa pale msamvu, igumbilo Iringa ndio hela ya mlo wa siku kwa mwingine.
- Nauli yako ya Mbeya - Mwanza unayotoa kwa kulalamika kwamba ni kubwa, ndiyo hela ya mwingine ya chai kila siku kwao.

**Mfano wa 01.** Cornel Harland Sanders wa KFC.

- Colonel Harland Sanders mwanzilishi wa migahawa ya KFC duniani alisota ujana wake wote akaja kutoka kimaisha akiwa mzee wa miaka 64 na kuacha jina lake kwenye kitabu cha mabilionea baada ya kufariki akiwa na umri wa miaka 90.




- 1. Akiwa na umri wa miaka mitano alifiwa na baba yake.
- 2. Akiwa na umri wa miaka 16 aliacha shule.
- 3. Akiwa na umri wa miaka 17 tayari alishafukuzwa kazi mara nne.

- 4. Akiwa na umri wa miaka 19 alikuwa mume wa mtu.
- 5. Akiwa na miaka 20 aliachwa na mke na watoto wake.
- 6. Akaomba kusoma sheria akanyimwa nafasi.
- 7. Akaingia kwenye biashara zikabuma.
- 8. Akaajiriwa kupika na kuosha vyombo kwenye mgahawa mdogo, akastaafu kazi hiyo akiwa na umri wa miaka 65, akapata mafao ya 250,000/=
- 9.Akaona serikali imemdharau sana.
- 10. Akajaribu kujiua ikashindikana.
- 11. Akaandika matarajio yake kwenye karatasi.
- 12. Akaangalia aliyoyakamilisha tayari, akagundua kuna mengi hakuyafanya bado.
- 13. Akagundua eneo moja ambalo anaweza kulifanya vizuri zaidi kuliko mtu yeyote ni kupika.
- 14.Akachukua 190,000/= kutoka kwenye mafao yake, akanunua kuku.
- 15. Akawakaanga kwa viungo murua.
- 16. Akapita nyumba kwa nyumba, kuwaza kwa majirani zake huko Kentucy.
- 17. Chakula hicho kikapendwa sana.




- 18. Akaamua kuanzisha mgahawa wake wa Kentucy Fried Chicken (KFC).

- 19. Biashara ikakua na akafungua migahawa mingine mingi ya KFC nchini Marekani.
- 20. Kwa sasa migahawa ya KFC imeenda kote duniani, ikiwemo Tanzania.
- 21. KFC ni mgahawa wa pili mkubwa ulioenea zaidi duniani baada ya migahawa ya mcdonald.
- 22. Alikufa ni bilionea akiwa na umri wa miaka 90.
- Simaanishi kama bado ni kijana utumie muda wa ujana wako kufanya mambo yasiyoeleweka kwa kudhania nawewe utafanikiwa uzeeni, alooo kumbuka UJANA MAPAMBANO na FAINALI UZEENI, anza kupambana ukiwa bado mdogo kwani hakuna mwenye uhakika wa kuiona kesho.




**A: UKIWA UNAJITAFUTA UTAKUWA PEKE YAKO.**

Mkulima akiwa shambani kupambania malengo yake, katika wakati huu hakuna atakae muuliza kuhusu chochote, lakini ikifika wakati wa mavuno na kula watu wengi watajitokeza kujenga ukaribu naye ili kufaidi jasho lake, tena ikitokea wamenyimwa watu hawa hunung'unika na kutangaza ati fulani mchoyo heeeeeh!

**B: SIKU UKIFANIKIWA WATU WATAKUSHANGILIA MFANO WA PICHA HII.**



Hakuna wakati ambao utajihisi unapendwa sana kama wakati wa mafanikio yako, kwani kila mtu ataonesha kukukimbilia, kukupongeza na kukusapoti, lakini ndio wakati ambao unatakiwa kuwa makini sana, kwani katika hao watakaokuonesha nyuso za tabasamu na furaha juu ya mafanikio yako basi tegemea kundi kubwa lipo kinyume na lipo hapo kutafuta namna nzuri ya kukuangamiza na kukushusha kaisa.

**Mafanikio ni mchakato wa muda mrefu lakini kushuka ni jambo la dakika moja. Kuwa makini mtu wangu.**

**Naamini umejifunza kitu kipya kupitia kitabu hiki, ahsante kwa zawadi yako ya Muda na fedha, hakika havijaenda bure na Mungu wa mbinguni akubariki sana.**

**KUWA KARIBU NAMI KUPITIA MITANDAO YANGU YA KIJAMII.**

Ili kupata Makala za kufundisha na kuelimisha.

**Facebook:** SUPERSTONE CHIDEBE II

**Instagram:** SUPERSTONE95

**Tik tok:** SUPERSTONE 99

Barua pepe: livingstonemusa761@gmail.com

Kupata kitabu changu hiki cha kwanza cha **NJIA NILIZOPITA.**

**Nakala laini (soft copy)** tembelea website ya Get Value: https://www.getvalue.co/prod/njia_nilizopita_02.


**Nakala ngumu (hard copy):** wasiliana na timu yetu ya mauzo kwa namba:

**0715374445** - YAS (TIGO)

**0782639761** – AIRTEL

**0621669761** – HALOTEL

**SASA KANUNUE KITABU CHOTE UPATE MENGI MIONGONI MWA HAYA MACHACHE.**





Livingstone Musa ni mtanzania, ni Afisa masoko kitaaluma, taaluma aliyoipatia katika chuo cha kikatoliki Mbeya Catholic University of Mbeya (CUoM) 2024.

## KUHUSU UANDISHI

Ni mwandishi wa vitabu, hadi sasa amefanikiwa kuandika vitabu viwili: Njia nilizopita pamoja na Mifumo ya mafanikio.

Ni mkurugenzi wa Stoney Products inayojihusisha na suala zima la usambazaji vitabu na huduma nyingine. Ni mwasisi wa Friend's love Charity foundation taasisi ambayo bado haijasajiliwa rasmi lakini ipo mbioni kusajiliwa.

Shauku yake kubwa ni kuweza kuambukiza watu wengi maarifa yenye kuwainua kiuchumi pamoja na kijamii. Hivyo hutumia jukwaa la mitandao ya kijamii kuweza kupanda mbegu njema kwa njia ya makala nzuri na za kuvutia.

Superstone Chidebe II
Superstone95
Superstone 99

ISBN 978-9912-42-725-9
9 789912 427259